

Maswali

1. Ni jinsi gani Abramu na Lutu walipata kuwa matajiri?
2. Kadiri mifugo na wanyama walivyoongezeka, siku zote walikuwa wakitafuta nini?
3. Wachungaji wa Abramu na Lutu walifanya nini, walipokosa malisho na maji?
4. Abramu alifanya nini kilichoonyesha kwamba alikuwa mtu mwema?
5. Ni sehemu gani ya nchi ya Kanaani aliyoichagua Lutu?
6. Ni kwa sababu gani Mungu aliendelea kumbariki Abramu?
7. Mungu alimwahidi nini kwamba atampa Abrahamu?
8. Abrahamu atapewa lini nchi alivyoahidiwa zamani za kale?

Majibu

1. Abramu na Lutu walikuwa tajiri wa kondoo na mbuzi.
2. Mifugo na wanyama walivyoongezeka walikuwa wakitafuta malisho na maji.
3. Wachungaji walipokosa malisho na maji waligombana.
4. Abramu alionyesha wema wake alipomwambia Lutu awe wa kwanza kuchagua upande apendao.
5. Lutu alichagua kuenda kwenye Bonde la Mto wa Yordani.
6. Mungu aliendelea kumbariki Abramu kwa sababu alikuwa mwema na mkarimu.
7. Mungu aliahidi Ibrahimu nchi ya kanaani na wazao wengi.
8. Ibrahimu atapewa hiyo nchi wakati wa ufalme wa Mungu duniani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awama ya 1 Mwaka wa 1

6 Abramu na Lutu

Marejeo

Mwanzo 13

Kiini cha somo

Kuonyesha Abramu hakutaka kugombania pahali pazuri pa nchi. Aliiamini kwamba Mungu atamlinda na kuziweka zile ahadi.

Maneno maalum

1. Abramu, Sarai, Lutu + Kanaani + mifugo (wanyama).
2. Mifugo wengi + nyasi haba (kidogo) + pigana.
3. Abramu + Karimu + Lutu + mto Yordani.
4. Abramu + amini Mungu.
5. Mungu + ahadi + Abramu + ufalme wa Mungu

6.1 Abramu, Sarai na Lutu waliishi katika nchi ya Kanaani, nchi aliyoagiza Mungu. Watu walioishi katika nchi, Wakanaani, walikuwa watu wakali na washupavu. Abramu na Lutu walikaa pamoja nao. Walikuwa na watumwa wengi wa kuangalia mifugo yao. Naye Mungu aliwabariki.

6.2 Baada ya miaka mingine kupita, wote wawili Abramu na Lutu wakawa matajiri. Walikuwa na wanyama na mifugo mingi. Wakiwa na wanyama wengi ikawa shida kupata malisho ya kutosha na maji kwa ajili yao wote. Hali ikawa mbaya sana. Wachungaji wa Abramu na Lutu wakaanza kushindana na kupigania malisho na maji. Mapigano yakazidi kuwa mabaya siku hadi siku. Hatimaye Abramu na Lutu wakakata shauri kwamba itakuwa vizuri wao wakitengana. Waliamua kuelekea njia tofauti ili kupata nyasi nzuri na kuchimba visima vipyta ya maji.

6.3 Abramu alikuwa na umri mkubwa kuliko Lutu. Angekuwa wa kwanza kufanya uamuzi kuhusu njia ya kwenda. Abramu alikuwa mwema na mkarimu. Akampa Lutu awe wa kwanza kuchagua. Abramu na Lutu wakapanda juu ya kilima. Toka kileleni waliweza kuona nchi yote hadi sehemu ya mbali. Lutu akatazama kwenye Bonde la Mto Yordani. Huo Mto ulifanya malisho kuwa mazuri na ya kijani. Kulikuwa na maji tele na pia kulikuwa na miji kadhaa katika bonde ambako Lutu aliweza kupata marafiki.

Ndipo Lutu alitazama upande mwingine. Haukuwa na mto. Itakuwa ni kazi ngumu kuchimba visima ili kupata maji. Vilima havikuwa na mto. Itakuwa ni kazi ngumu kuchimba visima ili kupata maji. Vilima havikuwa na majani mengi. Upande wa pili kulikuwa na jangwa. Hakuna kilichomea jangwani. Lutu akachagua Bonde Yordani. Lutu alifurahi sana kwakuwa alichagua eneo kama hilo zuri kwa kuishi. Akawa na maji tele na malisho kwa mifugo yake. Kulikuwa na miji ambako aliweza kupata marafiki.

6.4 Abramu alikuwa na furaha kwa nchi aliyoikaa. Alijua kwamba watu walioishi kwenye Bonde la Yordani walikuwa wabaya sana. Abramu hakutaka kufanya urafiki na watu wakaidi, Abramu alikuwa rafiki wa Mungu. Abramu hakujali kazi ngumu kiasi gani kutunza wanyama wake. Abramu hakuwa na wasi wasi ya kwamba hapakuwa na malisho ya kutosha. Alijua kwamba Mungu atamtunza. Mungu akafanya ahadi nyingine kwa Abramu.

6.5 Mungu alifanya ahadi nyingine na Abramu. Mungu alimwambia Abramu atazame toka pale alipo juu ya kilima. Alitazama pande zote umbali aliweza kufikisha macho yake. Mungu alimwahidia kumpa Abramu nchi hiyo. Yote, pamoja na Bonde la Yordani. Mungu atampa Abramu nchi yote ya Kanaani milele.

Mungu alimwambia ashuke chini ya mlima na kutembea katika nchi yote aweze kuiangalia. Mungu atampa nchi hiyo milele. Mungu alirudia ahadi ileile aliyoifanya hapo kabla. Mungu alimwahidi Abramu atakuwa na watoto wengi hata itakuwa vigumu kuwahesabu. "Huwezi kuhesabu punje za mchanga ulioko pwani ya ziwa," alisema Mungu, "wala hutaweza kuhesabu watoto wako, kwa kuwa watakuwa wengi mno."

Abramu aliishi nchi ya Kanaani maisha yake yote hadi mwisho. Lakini kamwe hakupewa kipande chochote ndani yake. Sarai mkewe alipokufa, hakuwa na sehemu yo yote ya ardhi kwa kuzikia, basi ikambidi anunue kipande kidogo cha ardhi kwa ajili ya kuzikia na hivyo akamzika Sarai mkewe. Hata hakuwahi kupewa nchi ya kutosha kuweka uwayo wa mguu wake!

Je! Mungu alisahau ahadi yake kwa Abramu?

La Siku zote Mungu anatunza ahadi zake. Mapema Yesu atarudi duniani. Yesu atamfufua Abramu katika wafu. Ndipo atapewa hiyo nchi. Abramu ataiishi katika Ufalme wa Mungu duniani milele.

